# HALMASHAURI YA WILAYA YA GAIRO

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI MDOGO WA HALMASHAURI YA WILAYA GAIRO MNAMO TAREHE 20/12/2021**

**Wajumbe waliohudhuria:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Isaya Mihinzo | Mwenyekiti |
| 2. | Salima Rajabu | Katibu |
| 3. | Dr. Godbless E. Luhanga | Mjumbe |
| 4. | Eunice M. Kyungay | Mjumbe |
| 5. | Adv. Waryoba Mussa | Mjumbe |

**Wajumbe wasiohudhuria:**

1. Nurath Hussein - Kwa taarifa
2. Nivoneia E. Levery - Kwa taarifa

**Wajumbe waalikwa:**

1. QS. Boniface Chama

**Sekretarieti:**

1. Mansur Mwakalinga

**AGENDA**

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Majukumu ya wajumbe wa Bodi ya Zabuni
4. Kusoma muhtasari wa tarehe 12/10/2021
5. Kuridhia njia ya manunuzi, tangazo na nyaraka za zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali.
6. Taarifa ya miradi iliyoongezeka katika mpango wa manunuzi 2021/2022 kutoka shilingi 5,055,722,640.00 hadi shilingi 6,998,857,639.72
7. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti
8. Kufunga kikao

**AGENDA. NA TB/1/20/12/2021 - KUFUNGUA KIKAO.**

Katibu aliwasilisha agenda na kumkaribisha mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 4.15 asubuhi.

**AGENDA. NA.TB/2/20/12/2021 - KUTHIBITISHA AGENDA**

Jumla ya agenda saba (7) ziliwasilishwa na kuthibitishwa. Agenda hizo ni-

**AGENDA**

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Majukumu ya wajumbe wa Bodi ya Zabuni
4. Kusoma muhtasari wa tarehe 12/10/2021
5. Kuridhia njia ya manunuzi, tangazo na nyaraka za zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi mbalimbali.
6. Taarifa ya miradi iliyoongezeka katika mpango wa manunuzi 2021/2022 kutoka shilingi 5,055,722,640.00 hadi shilingi 6,998,857,639.72
7. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti
8. Kufunga kikao

**AGENDA. NA.TB/3/20/12/2021: Majukumu ya wajumbe wa Bodi ya Zabuni**

Katibu aliwasilisha agenda na kutoa maelezo yanayohusiana na majukumu mbalimbali ya wajumbe wa bodi ya zabuni ambayo yapo kulingana na matakwa ya sheria ya ununuzi wa umma ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013 na sheria ya Serikali Mitaa ya Fedha ya mwaka 2018.

Baada ya maelezo Mjumbe aliunga mkono hoja kwa kusema ni vyema katibu akaelezea angalau kwa uchache juu ya majukumu hayo ya wajumbe wa bodi ya zabuni ili kila mmoja awe na uwelewa juu ya majukumu yao.

Katibu alibainisha kuwa majukumu kama ifuatavyo:-

- Kuridhia njia ya kufanya manunuzi
- Kupitia mapendezo ya kamati ya tathmini ya zabuni
- Kuridhia gharama za nyongeza katika miradi
- Kuridhia nyaraka za zabuni na mikataba
- Kuridhia mpango wa manunuzi wa mwaka
- Kutoa tuzo kwa kazi mbalimbali.

Mwenyekiti alielekeza kuwa zitolewe nakala za majukumu ya wajumbe wa bodi ya zabuni ili wapatiwe wajumbe wote ili wajue majukumu yao.

**AGENDA. NA.TB/4/20/12/2021: Kusoma muhtasari wa tarehe 12/10/2021**

Katibu aliwasilisha agenda na kutoa maelezo kuwa mnamo tarehe 12/10/2021 kilifanyika kikao cha robo ya kwanza (Julai – Septemba, 2021) hivyo umewasilishwa kwa ajili ya kuhakiki kama yalizungumzwa ndiyo yaliyoandikwa. Wajumbe waliupitia muhtasari huo na kuuthibitisha kuwa ni muhtasari sahihi na kusainiwa.

**AGENDA. NA.TB/5/20/12/2021: KURIDHIA NJIA YA MANUNUZI, TANGAZO NA NYARAKA ZA ZABUNI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA KAZI MBALIMBALI**

Katibu aliwasilisha agenda na kutoa maelezo kuwa miradi/kazi mbalimbali ambazo zinatakiwa kutekelezwa kwa kutumia njia mbali mbali za manunuzi, ambapo miradi itatekelezwa kupitia mpango maalumu wa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVICO – 19 kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka shirika la fedha duniani, fedha ya mapato ya ndani maendeleo na ukusanyaji wa mapato katika baadhi ya vyanzo na ununuzi wa vifaa.

Hata hivyo Katibu alitoa maelekezo kuwa kwa miradi ya UVICO – 19 (Afya) inabidi taratibu za kuwapata wakandarasi zifanyike hata hivyo Katibu alisoma barua ya maelekezo ya tarehe 25/11/2021 yenye Kumb.Na. AH.161/01/103 kutoka kwa Kaimu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yenye maelekezo mbalimbali ya kutekeleza miradi hiyo. Mchanganuo wa miradi kwa ujumla wake ni kama ifuatavyo:-

i. Fedha ya ujenzi wa vibanda vya kuchomea nyama – Unguroad shilingi 4,000,000.00
   - Njia ya manunuzi ni ushindani wa nukuu za bei kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi na kutumia mafundi (Local Fundi's) – "Force Account".

ii. Fedha ya kutengeneza maegesho ya malori shilingi 18,000,000
   - Njia ya manunuzi ni ushindani wa nukuu wa bei kwa kutumia mkandarasi.

iii. Fedha ya kununua mashine 6 za kufyatulia tofari za inchi sita shilingi 3,000,000.00
   - Njia ya manunuzi ni ushindani wa nukuu wa bei.

iv. Fedha ya kununua mashine ya kutengeneza chaki shilingi 5,500,000.00
   - Njia ya manunuzi ni ushindani wa nukuu wa bei

v. Fedha ya kununua vifaa vya kutengeze sabuni shilingi 6,935,000.00
   - Njia ya manunuzi ni ushindani wa nukuu wa bei.

vi. Kuridhia Tangazo la zabuni na nyaraka za zabuni kwa ajili ya huduma ya kufanya usafi, Kuzoa taka ngumu na Kukusanya Ada ya Usafi & Kukodisha Kantini ya Halmashauri ambapo gharama ya tangazo ni shilingi 826,000.00.
   - Njia ya manunuzi ni ushindaji wa Kitaifa kwa kutangaza katika gazeti la serikali (Habari Leo).

vii. Fedha ya makisio ya makusanyo ya ada ya usafi, kufanya usafi, kuzoa taka ngumu makisio shilingi 28,000,000.00 kwa mwaka.
   - Njia ya manunuzi ni ushindani wa Kitaifa kwa kutangaza katika gazeti la serikali.

viii. Fedha ya ujenzi wa nyumba ya mtumishi moja (Tatu kwa moja) shilingi 90,000,000.00 zabuni namba LGA/143/2021/2022/BL/W/02.
   - Njia ya manunuzi ni ushindani kwa utoaji wa zabuni ulio na utaratibu maalum (Restricted method) kwa maana kuwapatia nyaraka za zabuni Taasisi za Serikali na wakandarasi wenye sifa stahiki kulingana na kazi zilizoainishwa ambao ni wakandarasi wa majengo na watapatikana katika tovuti ya Bodi ya wakandarasi.

ix. Fedha ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura (Emergence Medical Department) shilingi 300,000,000.00 zabuni namba LGA/143/2021/2022/BL/W/01.
   - Njia ya manunuzi ni ushindani kwa utoaji wa zabuni ulio na utaratibu maalum (Restricted method) kwa maana kuwapatia nyaraka za zabuni Taasisi za Serikali na wakandarasi wenye sifa stahiki kulingana na kazi

- zilizoainishwa ambao ni wakandarasi wa majengo na watapatikana katika tovuti ya Bodi ya wakandarasi.

x. Fedha za ujenzi wa madarasa hamsini na tano katika Shule za sekondari kumi na nne yenye jumla ya shilingi 1,100,000,000.00.
   - Njia ya manunuzi ni "Force Account".

xi. Fedha za ujenzi wa vyumba vya Madarasa katika Shule Shikizi ya Magenge yenye jumla ya shilingi 40,000,000.00.
   - Njia ya manunuzi ni "Force Account".

xii. Fedha ya Ujenzi wa Hosteli ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Ukwamani lenye gharama ya shilingi 80,000,000.00.
   - Njia ya manunuzi ni "Force Account.

xiii. Kuridhia Tangazo la zabuni na nyaraka za zabuni kwa ajili **ya** huduma ya kukodisha kantini ya Halmashauri. Njia ya manunuzi ni ushindaji wa Kitaifa kwa kutangaza katika gazeti la serikali (Habari Leo).
Makisio ya fedha ya kukodisha kantini ni shilingi 300,000.00 kwa miezi sita.

xiv. Fedha ya ujenzi wa sekondari ya Leshata katika Kata ya Leshata shilingi 600,000,000.00 kwa kutumia fedha ya kuboresha elimu ya sekondari Nchini (SEQUIP).Awali mradi huu ulishaingia katika mpango wa manunuzi wa mwaka fedha 2021/2022 na njia ya manunuzi ilikuwa "Force Account". Hata hivyo kwa kurejea maelekezo ya utekelezaji wa miradi ya (SEQUIP – Secondary Education Quality Improvement Program) ambayo nayo inagharamiwa na Serikali kwa mkopo wa Takribani shilingi Trioni 1.1 toka Benki ya Dunia, njia ya manunuzi inayoweza kutumika ni "Force Account".

Kutokana na maelekezo hayo wajumbe walijadili na kupendekeza njia ya "Force Account" kama ilivyoelekezwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka 2021/2022 itumike cha msingi majengo yawe na ubora hii ni kutokana na uhalisia wa fedha iliyopokelewa.Hivyo vifaa vinunuliwe na ushindani wa kazi za ujenzi ufanyike kwa kuwatumia wakandarasi binafsi wa majengo au Taasisi za Serikali zinazoshughulika na ujenzi wa majengo au "local fundi's" ambaye kweli anajua kazi ambapo Kamati ya ujenzi itamfanyia tathmini ya kina.Hata hivyo pesa hizo zitapokelewa kwa awamu tofauti kwa maana kwa sasa fedha iliyopokelewa ni shilingi 470,000,000.00 na fedha kiasi cha shilingi 130,000,000.00 zitapokelewa baadae kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi wa sekondari katika Kata ya Leshata na baadae shule ya sekondari katika Kata nyingine ambapo gharama ya mradi pia ni shilingi 600,000,000.00 kwa kutumia njia hiyo hiyo ya manunuzi. Shule itakayojengwa itakuwa na uwezo

wa kuchukua wanafunzi wasiopungua 400 kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

Mradi wa SEQUIP umelenga kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya sekondari, kuweka mazingira salama ya elimu kwa wasichana na kuhakikisha wanafunzi wote wanapata elimu bora ya sekondari.

Baada ya kuwasilishwa taarifa hiyo Mjumbe aliwasilisha pendekezo juu ya Tangazo la Huduma ya Kantini ya Halmashauri na kushauri ni vyema kabla ya kutangaza ifanyike jitihada kwa Idara ya Utawala na Utumishi kukamilisha mtandao wa maji, umeme viwe vimetenganishwa na jengo la ofisi kuu pia vifaa vya uchaguzi vitafutiwe eneo la kuviweka kwa usalama.

Hata hivyo Mwenyekiti alimkaribisha mjumbe kutoka ofisi ya Ujenzi kwa ajili ya kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu agenda ya upatikanaji wa wakandarasi wa ujenzi kwenye utekelezaji wa miradi ya UVICO -19 ya Idara ya Afya. Mjumbe alielezea changamoto zilizopo za kutumia Taasisi za Serikali na kushauri kuwa ni vyema pia na wakandarasi wengine wenye sifa wakashindanishwa ili kuongeza ushindani ili ufanisi wa kazi uwe bora.Pia alisisitiza njia ya manunuzi iwe ya haraka ili mradi utekelezwe ndani ya miezi minne. Vilevile aliongezea kwa kusema hata Mhandisi wa Mkoa amesisitiza kuwa nyaraka za zabuni tusiwape Taasisi za Serikali peke yake.

Pia mjumbe alichangia hoja kuhusu kutangazwa kwa zabuni ya uzoaji taka kuwa mzabuni yeye aseme atatakulipwa asilimia ngapi ambayo itahusisha gharama za uendeshaji na faida yake.

Baada ya majadiliano hao wajumbe walijadili na kuridhia utekelezaji wa miradi hiyo sambamba na njia zake za manunuzi, tangazo na nyaraka za zabuni.

**AGENDA. NA.TB/6/20/12/2021: KUPITIA NA KUHUISHA MPANGO WA MANUNUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KUTOKA SHILINGI 5,055,722,640.00 HADI SHILINGI 6,998,857,639.72**

Katibu aliwasilisha agenda na kutoa maelezo kuwa mpango wa manunuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wa Halmashauri ya wilaya ya Gairo ulikuwa na manunuzi yenye jumla ya shilingi 5,055,772,640.00. Hata hivyo mpango huo wa manunuzi unatakiwa kuhuisha kwasababu ya kuongezeka kwa kazi baada ya kupokea fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo kupitia mpango maalum wa "Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO – 19" kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha Dunia zilizo nje ya bajeti 2021/2022, fedha ya mapato ya ndani maendeleo na ukusanyaji wa mapato katika baadhi ya vyanzo na ununuzi wa vifaa. Katibu alielezea kuwa miradi/kazi hizo za nyongeza zinajumuisha miradi ifuatayo:-

(1).Fedha ya ujenzi wa vibanda vya kuchomea nyama – Unguroad shilingi 4,000,000.00

(2). Fedha ya kutengeneza maegesho ya malori shilingi 18,000,000

(3). Fedha ya kununua mashine 6 za kufyatulia tofari za inchi sita shilingi 3,000,000.00

(4). Fedha ya kununua mashine ya kutengeneza chaki shilingi 5,500,000.00

(5). Fedha ya kununua vifaa vya kutengeze sabuni shilingi 6,935,000.00

(6). Makisio ya fedha ya kukusanya ada ya usafi shilingi 28,000,000 kwa mwaka.

(7). Makisio ya fedha ya kukodisha kantini shilingi 300,000.00 kwa miezi sita.

(8). Fedha ya ujenzi wa nyumba ya mtumishi moja (Tatu kwa moja) shilingi 90,000,000.00.

(9). Fedha ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura (Emergence Medical Department) shilingi 300,000,000.00.

(10). Fedha za ujenzi wa madarasa hamsini na tano katika Shule za sekondari kumi na nne shilingi 1,100,000,000.00.

(11). Fedha za ujenzi wa vyumba vya Madarasa katika Shule Shikizi ya Magenge shilingi 40,000,000.00.

(12). Fedha ya Ujenzi wa Hosteli ya wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Ukwamani shilingi 80,000,000.00

(13). Fedha za Ujenzi Kituo cha Afya Kata ya Nongwe Wilayani Gairo shilingi 250,000,000.00 ambayo ni gawio la tozo za simu.

(14) Fedha za Tasaf zitakazotumika katika manunuzi kiasi cha shilingi 17,400,000.00 kwa mchanganuo ufuatao:-

i. Ununuzi wa mafuta diseli shilingi 10,080,000.00
ii. Ununuzi wa shajala shilingi 3,720,000.00
iii. Ununuzi wa huduma ya matengenezo ya magari shilingi 3,600,000.00

Wajumbe walijadili na kuridhia ongezeko la bajeti kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka 2021/2022 kutoka **5,055,722,640.00 hadi shilingi 6,998,857,639.72.**

Pia wajumbe waliridhia mabadiliko ya matumizi ya fedha ya shilingi 500,000,000.00 ya ujenzi wa Kituo cha Afya Nongwe kwenda kufanya ujenzi wa Kituo cha Afya Iyogwe hii ni kutokana na mapokezi ya fedha ya shilingi 250,000,000.00 ya tozo za simu kwenda Nongwe kujenga Kituo cha Afya.

**AGENDA. NA.TB/7/20/12/2021: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili aongee machache. Ndipo Mwenyekiti alisema amepokea mengineyo kutoka kwa mjumbe mmoja ambaye hoja yake ilikuwa kujua stahiki za wajumbe wa Bodi ya zabuni.

Katibu alijibu hoja hiyo kama ifuatavyo:

i. Wajumbe wa Bodi ya zabuni wanatakiwa kulipwa posho ya kikao kwa mchanganuo ufuatao: Mwenyekiti na Katibu kila mmoja shilingi 200,000.00, wajumbe watano kila mmoja shilingi 150,000.00, sekretarieti mmoja shilingi 100,000.00 na mwalikwa itategemeana na bajeti.
ii. Wajumbe wanahaki ya kuhudhuria mafunzo, semina kutokana na bajeti ya Halmashauri inaporuhusu ili kupata ufahamu wa kuhusu sheria mbalimbali zinazohusu manunuzi.

Pia Katibu alizungumzia juu ya bajeti ya kitengo cha manunuzi na namna ya ulipaji wa posho hizo, alieleza jinsi gani anavyofanya juhudi ili wajumbe walipwe lakini hoja kuu za wajumbe ni kuwa mbona vikao vingine kama vile Bodi ya Ajira, vikao vya kamati ya ukaguzi vinalipwa? Ila vikao vya bodi ya zabuni havilipwi?. Katibu alijibu kuwa changamoto ni ofisi ya Mkurugenzi kwasababu vikao vyote bajeti yake ipo katika vifungu vya kulipia vikao vya Halmashauri na si vinginevyo.

Hata hivyo Katibu alisisitizwa na wajumbe kuandaa dokezo la posho kwa kajili ya kikao kijacho.Katibu pia alitoa maelezo kuhusu kazi ya tathmini ya miradi ya Uvico -19 na kushauri kuwa ofisi ya Mkurugenzi ni vyema iandike barua kwa Katibu Tawala wa Mkoa na ofisi ya TARURA ili wapatikane wataalamu wa kufanya kazi hiyo kwa kushirikiana na wataalam toka Halmashauri.

**AGENDA. NA.TB/8/20/12/2021: KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuchangia hoja mbalimbali katika kikao. Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 1.05 mchana.

**MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA NA KUTIWA SAINI NA:-**

| | |
|---|---|
| Isaya Mbuinzo | Salum Rajab |
| (JINA LA MWENYEKITI) | (JINA LA KATIBU) |
| [signature] | [signature] |
| SAINI | SAINI |
| 07/01/2022 | 7/1/2022 |
| TAREHE | TAREHE |